**HALMASHAURI YA MANISPAA YA KAHAMA**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 – ROBO YA NNE

## Bajeti ya Miradi

Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Halmashauri ya Manispaa iliidhinishiwa kiasi cha Shs. 13,559,260,240.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mchanganuo ufuatao Shs. 8,705,962,000.00 (64.21%) kwa ajili ya miradi ya maendeleo kutokana na fedha za Ruzuku na Wahisani, kiasi cha Shs. 4,853,298,240.00 (35.79%) kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kwa Fedha za Mapato ya Ndani. Fedha za Bakaa kwa Mwaka 2022/2023 ni Shs. 606,189,917.38. Aidha Halmashauri ina kiasi cha Shs. 1,604,000,000.00 za CSR VB (Receipt in Kind) kwa ajili ya Miradi inayoendelea na utekelezaji kwa Mwaka 2023/2024.

## Fedha zilizopokelewa kwa ajili ya Miradi kuanzia Machi 2023 hadi Juni, 2024

Kuanzia Mwezi Julai 2023 hadi Juni, 2024 kiasi cha Shs. 14,356,342,727.49 (106%) kimepokelewa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo katika mchanganuo ufuatao: Ruzuku kutoka Serikali Kuu na Wahisani Shs. 9,503,044,487.49 (109.16%), Shs. 4,853,298,240.00 (100%) Mapato ya Ndani na Bakaa Shs 606,189,917.38.

## Miradi ya Maendeleo Mapato ya Ndani.

Makisio ya Fedha za Mapato ya Ndani kwa Mwaka 2023/2024 yalikasimiwa Shs. 4,853,298,240.00. Kiasi hiki cha fedha kimepelekwa kwenye miradi ya Maendeleo kwa asilimia 100 yaani ni Shs. 4,853,298,240.00 na zimegawanyika katika mchanganuo ufuatao:

| | | |
|---|---|---|
| • Miradi ya Maendeleo | Shs. | 4,082,933,440.00 |
| • Mfuko wa Maendeleo (Wanawake, Vijana na W/Ulemavu) | Shs. | 770,364,800.00 |
| **Jumla.........................................................** | **Shs** | **4,853,298,240.00** |

## Mfuko wa Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu

Katika Mwaka 2023/2024 Halmashauri ilikisia Shs. 770,364,800.00 ikiwa ni asilimia 10 ya Mfuko wa Wanawake, Vijana na Wenye ulemavu. Fedha iliyotolewa mpaka Mwezi Juni, 2024 kwenye Mfuko wa Wanawake, Vijana na Wenye Ulemavu ni Sh. 770,364,800.00 (100%). Kwa kipindi cha Mwezi Julai 2023 hadi Juni, 2024 hakuna mikopo iliyotolewa kwa vikundi kutokana na Serikali kusitisha zoezi hili kwa Halmashuri zote nchini kwamba zisitoe Mikopo hadi pale Mwongozo na Taratibu mpya za utoaji Mikopo zitakapoelekeza.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Jedwali lifuatalo linafafanua hali halisi ya mapokezi ya Fedha za miradi ya Maendeleo kwa vyanzo vyote kuanzia Julai 2023 hadi Juni, 2024.

**Jedwali Na. 1: Mapato ya Fedha za Miradi Julai 2023 hadi Juni, 2024**

| Na | Mradi | Bajeti 2023/2024 | Mapato Julai, 2023 hadi Juni, 2024 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Ndani Miradi | 4,853,298,240.00 | 4,853,298,240.00 | 100.0 |
| 2 | Tanzania Social Action Fund(TASAF) | 1,199,552,000.00 | 1,139,596,887.00 | 95.0 |
| 3 | Mfuko wa Pamoja wa Afya(HSBF) | 404,647,000.00 | 549,597,000.00 | 135.8 |
| 4 | UNICEF | 32,291,000.00 | 2,500,000.00 | 7.7 |
| 5 | Mfuko wa Jimbo | 77,510,000.00 | 77,510,000.00 | 100.0 |
| 6 | Secondary Education Quality Improvement –( SEQUIP) | 573,000,000.00 | 1,442,781,126.00 | 251.8 |
| 7 | Global Fund | 9,141,000.00 | 0.00 | 0.0 |
| 8 | Global Alliance for Vaccine and Immunization (GAVI) | 129,922,000.00 | 77,804,045.00 | 67.5 |
| 9 | Ruzuku ya Ndani Miradi | 1,188,000,000.00 | 2,440,200,000.00 | 205.4 |
| 10 | Nutrional International | 2,632,000.00 | 0.00 | 0.0 |
| 11 | Elimu Bila Malipo ( EBM) | 1,990,621,000.00 | 2,078,758,429.49 | 104.4 |
| 12 | P4R (BOOST) | 1,045,596,000.00 | 320,700,000.00 | 30.7 |
| 13 | THPS | 650,248,000.00 | 0.00 | 0.0 |
| 14 | M-MAMA | 29,205,000.00 | 0.00 | 0.0 |

| Na | Mradi | Bajeti 2023/2024 | Mapato Julai, 2023 hadi Juni, 2024 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 15 | MITIHANI ELIMU MSINGI NA SEKONDARI | 1,373,597,000.00 | 1,373,597,000.00 | 100.0 |
| | **JUMLA** | **13,559,260,240.00** | **14,356,342,727.49** | **106.0** |
| 16 | CSR VB (Receipt in Kind) | 1,604,000,000.00 | 420,701,920.00 | 26.2 |

## 2.0 Matumizi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai 2023 hadi Juni, 2024 Jumla ya Shs 12,667,423,019.50 (93.42%) zimetumika katika mchanganuo ufuatao; Shs 3,761,307,663.68 (77.50%) ya fedha zimetumika kwa upande wa Mapato ya Ndani katika kutekeleza miradi ya Maendeleo, Shs 8,906,115,355.82 (65.68%) fedha za Ruzuku na Wahisani zimetumika na Shs. 420,701,920.00 fedha za CSR.

Jedwali lifuatalo linaonyesha Matumizi yote ya Bajeti ya Miradi (Mapato ya Ndani na Ruzuku) kuanzia Julai 2023 hadi Juni, 2024.

**Jedwali Na. 1: Matumizi ya Fedha za Miradi Julai 2023 hadi Juni, 2024**

| Na | Mradi | Bajeti 2023/2024 | Matumizi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Ndani Miradi | 4,853,298,240.00 | 3,761,307,663.68 | 77.50 |
| 2 | Tanzania Social Action Fund(TASAF) | 1,199,552,000.00 | 2,710,157,890.00 | 225.93 |
| 3 | Mfuko wa Pamoja wa Afya(HSBF) | 404,647,000.00 | 599,584,397.00 | 148.17 |
| 4 | UNICEF | 32,291,000.00 | 2,500,000.00 | 7.74 |
| 5 | Mfuko wa Jimbo | 77,510,000.00 | 47,471,400.00 | 61.25 |
| 6 | Secondary Education Quality Improvement ( SEQUIP) | 573,000,000.00 | 815,124,563.00 | 142.26 |
| 7 | Global Fund | 9,141,000.00 | 11,932,535.61 | 130.54 |
| 8 | Global Alliance for Vaccine and Immunization (GAVI) | 129,922,000.00 | 57,748,038.00 | 44.45 |

| Na | Mradi | Bajeti 2023/2024 | Matumizi Julai, 2023 hadi Juni, 2024 | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 9 | Ruzuku ya Ndani Miradi | 1,188,000,000.00 | 1,690,042,202.21 | 142.26 |
| 10 | Nutrional International | 2,632,000.00 | 0 | 0.00 |
| 11 | Elimu Bila Malipo ( EBM) | 1,990,621,000.00 | 1,494,216,456.00 | 75.06 |
| 12 | P4R (BOOST) | 1,045,596,000.00 | 10,372,380.00 | 0.99 |
| 13 | THPS | 650,248,000.00 | 92,816,494.00 | 14.27 |
| 14 | M-MAMA | 29,205,000.00 | 552,000.00 | 1.89 |
| 15 | MITIHANI ELIMU MSINGI NA SEKONDARI | 1,373,597,000.00 | 1,373,597,000.00 | 100.00 |
| | **JUMLA** | **13,559,260,240.00** | **12,667,423,019.50** | 93.42 |
| 16 | CSR VB (Receipt in Kind) | 1,604,000,000.00 | 420,701,920.00 | 26.23 |

**NB: Kiasi cha Shilingi 1,152,314,407.00 Fedha za TASAF zimeingizwa moja kwa moja kwenye Akaunti za wanufaika**

## 3.0 Jedwali la Muhtasari wa Miradi ya Bakaa iliyotekelezwa 2022/2023

| Jina la mradi | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| **Mapato ya Ndani** | | | | |
| Ujenzi wa barabara ifikapo Juni 2024 | 555,227,020.51 | 555,227,020.51 | 414,471,984 | Awamu ya kwanza ya mradi km 0.36 umekamilika ambapo jumla ya kiasi cha shilingi 400,000,000 kimetumika . Awamu ya pili ya mradi yenye mkataba wa Shs.897,728,565.00 (km 1.03) kiasi cha Shs.414,471,983.79 kimetumika .Ujenzi unaendelea kwa kazi ya |

| Jina la mradi | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | kuweka tabaka la changarawe, ujenzi wa mitaro na vivuko.. |
| **Ruzuku Serikali Kuu Fedha za Ndani** | | | | |
| Ujenzi wa uzio wa Mabweni shule ya Msingi Mwime ifikapo June 2024 | 30,000,000 | 30,000,000 | 27,965,000 | Ujenzi wa uzio unaendelea. Fedha pokelewa haijatosheleza kukamilisha ujenzi wa uzio |
| **CSR (BUZWAGI)** | | | | |
| Ukamilishaji wa madarasa 2 Igomelo Shule ya Msingi | 32,000,000.00 | 32,000,000.00 | 32,000,000.00 | Madarasa yamekamilika na yanatumika |
| Ukamilishaji wa matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Seeke(Kadwini) | 12,500,000.00 | 12,500,000.00 | 12,500,000.00 | Mradi umekamilika na unatumika |
| Ukarabati wa matundu 10 ya vyoo Shule ya Msingi Ilindi (Kadete) | 10,500,000.00 | 10,500,000.00 | 10,500,000.00 | Mradi umekamilika na unatumika |
| Ukamilishaji wa madarasa 3 Shule Shule ya Msingi Kitwana | 49,500,000.00 | 49,500,000.00 | 49,500,000.00 | Mradi umekamilika na unatumika |
| Ukamilishaji wa madarasa 2 Shule ya Msingi Igunghwa | 33,000,000.00 | 33,000,000.00 | 33,000,000.00 | Mradi umekamilika na unatumika |
| Ununuzi wa Madawati 794 katika Shule za Msingi | 63,517,500.00 | 63,517,500.00 | 63,517,500.00 | Madawati yamenunuliwa |

| Jina la mradi | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| Ukamilishaji wa Jengo la OPD Zahanati ya Nuja | 25,000,000.00 | 25,000,000.00 | 25,000,000.00 | Ukamilishaji wa jengo la OPD umekamilika na umeme umeshafungwa, na choo kinaendelea na ukamilishaji. |
| **RUZUKU SERIKALI KUU** | | | | |
| Kuendeleza Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Manispaa Kahama ifikapo Juni 2024 | 500,000,000.00 | 500,000,000.00 | 500,000,000.00 | Mradi huu ni endelevu utekelezaji upo hatua ya kufunga nguzo ghorofa ya kwanza. Jumla ya fedha iliyotumika ni Shs. 1,947,087,751.27 (Ruzuku S/Kuu Shs. 1,247,824,075.39) na Mapato ya Ndani Shs. 699,254,675.88).Mradi unatarajiwa kukamilika tarehe 15 Juni 2025 . Jumla ya fedha pokelewa mpaka sasa ni Shs. 2,700,000,000.00 (Ruzuku Shs. 1,500,000,000 na Mapato ya Ndani Shs. 1,200,000,000.00). |
| Kuwezesha ununuzi wa vifaa Tiba katika Hospitali ya Manispaa | 250,000,000.00 | 250,000,000.00 | 250,000,000.00 | Vifaa tiba vimenunuliwa na kupelekwa vituoni. |

| Jina la mradi | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| Kahama,Kituo cha Afya Kagongwa, Kituo cha Afya Nyashimbi, Kituo cha Afya Kinaga ifikapo Juni 2024 | | | | |
| **SEQUIP** | | | | |
| Ujenzi wa Shule Mpya ya Sekondari Kata ya Nyahanga. | 603,890,562.00 | 603,890,562.00 | 603,890,562.00 | Ujenzi umekamilika |
| Kusaidia jamii katika Ujenzi wa Nyumba 2 za Walimu katika Shule ya Sekondari Kagongwa | 110,000,000.00 | 110,000,000.00 | 110,000,000.00 | Ujenzi umekamilika |

### 3.1 Jedwali la Muhtasari wa Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa 2023/2024

| JINA LA MRADI | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| **Mapato ya Ndani** | | | | |
| **Shule za Msingi** | | | | |
| Ujenzi wa Madarasa 08 na ukamilishaji wa madarasa 05 katika Shule za Msingi | 230,000,000 | 230,000,000 | 230,000,000 | Ujenzi wa madarasa 08 na ukamilishaji wa madarasa 05 umekamilika |
| Ukamilishaji wa matundu 74 na ujenzi wa matuntu 12 ya vyoo katika shule za Msingi | 81,255,000 | 81,255,000 | 81,255,000 | Ujenzi na ukamilishaji umefanyika |

| JINA LA MRADI | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| Ukamilishaji nyumba 3 za walimu | 16,905,000 | 16,905,000 | 16,905,000 | Ukamilishaji wa nyumba 3 za walimu umefanyika |
| Utengenezaji wa madawati 4,648 Shule za Msingi | 371,840,000 | 371,840,000 | 100,000,000 | Madawati 2126 kati ya Madawati 4648 yamepelekwa shule |
| **Shule za Sekondari** | | | | |
| Ukamilishaji wa nyumba ya mwalimu Iyenze Sekondari | 13,248,000 | 13,248,000 | 13,248,000 | Nyumba imekamilika |
| Utengenezaji wa Viti na Meza 166 Shule za Sekondari | 13,280,000 | 13,280,000 | 13,280,000 | Jumla ya viti na meza 166 vimetengenezwa na kupelekwa mashuleni |
| **Sekta ya Afya** | | | | |
| Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Manispaa | 700,000,000 | 700,000,000 | 199,254,676 | Mradi huu ni endelevu utekelezaji upo hatua ya kufunga nguzo ghorofa ya kwanza. Jumla ya fedha iliyotumika ni Shs. 1,947,087,751.27 (Ruzuku S/Kuu Shs. |

| JINA LA MRADI | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | 1,247,824,075.39) na Mapato ya Ndani Shs. 699,254,675.88).Mradi unatarajiwa kukamilika tarehe 15 Juni 2025 . Jumla ya fedha pokelewa mpaka sasa ni Shs. 2,700,000,000.00 ( Ruzuku Shs. 1,500,000,000 na Mapato ya Ndani Shs. 1,200,000,000.00). |
| **Sekta ya Kilimo** | | | | |
| Kuwezesha uanzishaji wa mashamba darasa, shughuli za nanae kwa wagani na wakulima, pembejeo kwa wakulima, upembuzi wa awali wa mradi wa umwagiliaji Iyenze, chanjo za mifugo na mafunzo kwa wafugaji | 324,512,750 | 324,512,750 | 296,002,600 | uanzishaji wa mashamba darasa, shughuli za nanae kwa wagani na wakulima, pembejeo kwa wakulima, upembuzi wa awali wa mradi wa umwagiliaji Iyenze, chanjo za mifugo na mafunzo kwa wafugaji vimefanyika. Jumla ya wakulima 101 katika kata za Mondo na |

| JINA LA MRADI | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | Mwendakulima wamenufaika na pemebejeo. |
| **Maendeleo ya Jamii (Mikopo ya Asilimia 10)** | | | | |
| Asilimia 10 za wanawake vikundi 110, Vijana vikundi 110 na Watu wenye Ulemavu vikundi 53 katika kata 20 za Halmashauri | 770,364,800 | 770,364,800 | 0 | Fedha za Mikopo zimehamishiwa kwenye akaunti ya Mikopo |
| **Miundombinu na Uendelezaji Vijiji na Miji** | | | | |
| Ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami Km 1.39 | 770,364,800 | 770,364,800 | 0 | Awamu ya kwanza mradi umekamilika na shilingi 321,235,275.00 zimetumika. Awamu ya pili, ujenzi unaendelea kwa kazi ya kuweka tabaka la changarawe, ujenzi wa mitaro na vivuko ambapo kiasi cha shilingi 218,541,117.41 kimelipwa kwa Awamu ya pili. Jumla ya gharama ya mradi |

| JINA LA MRADI | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| | | | | ni Shs. 1,218.963,840.00 |
| Ufunguaji wa barabara mpya katika kata 20 | 300,000,000 | 300,000,000 | 300,000,000 | Barabara zimechongwa katika Kata 20 |
| Kuwezesha ulipaji wa fidia ya ardhi katika maeneo ya uwekezaji | 297,377,390 | 297,377,390 | 297,377,390 | Ulipaji wa fidia umefanyika katika maeneo ya uwekezaji |
| **Ruzuku Serikali Kuu Fedha za Ndani** | | | | |
| **Elimu ya Awali na Msingi** | | | | |
| Ukarabati wa vyumba 13 vya madarasa na ofisi 1, ujenzi wa uzio shule ya Watoto wenye mahitaji maalum Mwime na ujenzi wa matundu ya vyoo 32 katika shule za Msingi | 238,000,000 | 238,000,000 | 235,911,250.00 | Ukarabati umekamilika katika maeneo mengine kasoro S/M Nyahanga A, Guido, Buduba na Mwime ambapo kumekuwa na upungufu wa fedha. Maeneo haya yatakamilishwa kwa fedha za Mapato ya Ndani Mwaka 2024/2025 |
| **Elimu Sekondari** | | | | |
| Ujenzi wa Madarasa 37, ukamilishaji wa maboma 14 na ujenzi wa matundu | 1,252,200,000 | 1,252,200,000 | 1,113,870,700.00 | Ujenzi umekamilika. Madarasa na matundu ya vyoo |

| JINA LA MRADI | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| ya vyoo 64 ya Kidato cha Kwanza Mwaka 2023 | | | | vinatumika kasoro S/S Nyahanga ujenzi wa madarasa sita unaendelea na ukamilishaji |
| **Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe** | | | | |
| Kununua Vifaa Tiba katika Zahanati na vituo vya Afya, Kujenga Matanuru ya kuchomea Taka hatarishi na Mashimo ya kutupia kondo la nyuma katika Zahanati na kuendeleza Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Manispaa | 950,000,000 | 950,000,000 | 726,511,604 | Vifaa tiba vipo hatua ya manunuzi, matanuru na mashimo ya kondo la nyuma yapo hatua ya msingi na Jengo la Mama na Mtoto Hospitali ya Manispaa lipo hatua ya usukaji wa nondo na ufungaji viumbio kwa ajili ya sakafu kwenye ghorofa ya kwanza. |
| **Mfuko wa Jimbo** | | | | |
| Utekelezaji wa miradi ya mfuko wa jimbo | 77,510,000 | 77,510,000 | 47,471,400 | Vifaa mbalimbali vimepelekwa katika miradi iliyopendekezwa. |
| **Wahisani- Fedha za Nje** | | | | |
| Usimamizi wa huduma za Afya (Busket Fund), Fedha | | | | Usimamizi wa huduma za Afya |

| JINA LA MRADI | FEDHA IDHINISHWA | FEDHA TOLEWA | FEDHA TUMIKA | HATUA YA MRADI |
|---|---|---|---|---|
| za Kaya Maskini (TASAF) na SEQUIP | 4,076,234,000 | 4,685,293,465 | 4,300,788,297.61 | umefanyika na Fedha za kuhudumia kaya masikini zimetolewa, Miradi ya SEQUIP iliyotekelezwa ni Ujenzi wa nyumba ya Mwalimu Kagongwa Sekondari ,ujenzi wa Shule mpya Nyahanga Sekondari, ununuzi wa Viti na meza Nyahanga Sekondari, Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa Nyahanga, ukamilishaji wa Maabara 1 Isunuka Sekondari, ukamilishaji wa matundu 20 ya vyoo Kitwana Sekondari na Nyashimbi Sekondari |

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Majedwali ya michanganuo ya utekelezaji wa miradi yameambatishwa kwa rejea.

Naomba kuwasilisha,

Masudi Kibetu

**MKURUGENZI**

**MANISPAA YA KAHAMA**